# Mwongozo wa Familia kwa Huduma za Watoto za Mapema za NYS – Kabla ya Kuzaliwa hadi Miaka 5

Mwongozo wa huduma kwa familia kuungana na kuunganisha watoto kwenye huduma za watoto za mapema katika Jimbo la New York

## Home Visiting (kabla ya kuzaliwa hadi miaka 5)


Wageni wa nyumbani hutoa usaidizi kwa wanawake wajawazito na familia zilizo na watoto waliozaliwa hadi wa umri wa miaka 5 na kuendeleza ukuaji wa mtoto wenye afya. Ziara ya nyumbani inatolewa bila gharama kwa familia yako. Ili kupata mpango wa ziara ya nyumbani karibu nawe: **www.bit.ly/homevisitingnys**

**Mipango ya Home Visiting huunganisha familia kwenye huduma za jamii kama vile:**

- Huduma za Matibabu, Meno na Afya ya Akili
- Huduma ya Watoto
- Early Head Start na Head Start
- Huduma za Early Intervention
- Chakula, Nyumba na Ajira



## Huduma ya Watoto



(umri wa wiki 6 hadi miaka 12)

NYS Office of Children and Family Services (OCFS) inatoa maelezo kuhusu:

- kupata huduma
- kulipia huduma

Tovuti inajumuisha video na vijitabu na huduma za watoto za karibu na anwani za mawasiliano za shirika la rufaa.
**www.ocfs.ny.gov**

### QUALITYstarsNY (QSNY)

QSNY ni mfumo wa ukadiriaji ubora na uimarikaji wa NYS ili kuhakikisha kuwa watoto wachanga walio katika mipango ya huduma na elimu ya mapema wanapata ubora na familia zao zinaweza kuamini ubora wa mipango wanayochagua.

**www.qualitystarsny.org**



### Hatua za kuomba huduma kwa watoto

**1 Anza Mapema**
Kutafuta huduma sahihi ya mtoto kwa ajili ya familia yako kunaweza kuchukua muda fulani. Ni vizuri kutafuta hata ukiwa mjamzito. Unaweza kuangalia kwenye NYS Parent Portal li kupata huduma ya watoto kwenye: **www.nysparenting.org**

**2 Wasiliana na CCR&R Yako ya Karibu**
Wasiliana na Huduma za Watoto na Wakala wa Rufaa wa karibu kwa maelezo kuhusu mipango iliyo kwenye eneo lako. Orodha inaweza kupatikana kwenye tovuti ya OCFS katika:
**www.bit.ly/ChildCareReferral**

**3 Usaidizi wa Kulipia Huduma**
Je, unafahamu kwamba huenda ukastahiki kupata msaada wa kifedha ili kusaidia kulipia huduma ya watoto? Uliza CCR&R yako ya karibu kwa maelezo zaidi au nenda kwenye: **www.bit.ly/ChildCareFunds**

**4 Tembelea na Uulize Maswali**
Kutembelea ni njia bora ya kuamua kile kinachofaa mtoto na familia yako. Unda orodha ya kile ambacho ni muhimu kwako.

## Early Intervention

(miaka 0 hadi 3)

Kila kaunti ina Early Intervention Program (EIP) ya kusaidia watoto wachanga na wanaodema wa umri wa wakati wa kuzaliwa hadi miaka 3 walio na ulemavu au waliochelewa kukua. Huduma zinatolewa bila malipo kwa familia zinazostahiki. Pata mtoa huduma wa nchi yako kwenye:

**www.bit.ly/earlyinterventionnys**

**Rufaa**

Mwanafamilia au mtoa huduma aliwasiliana na Early Intervention Program.

**Mratibu wa Awali wa Huduma**

Mratibu anawasiliana na familia ili kushiriki maelezo kuhusu EIP.

**Tathmini**

Familia inakutana na mtoa huduma na kuamua ustahiki.

**Mkutano wa IFSP**

Ikiwa familia inastahiki, mpango ulioandikwa unaundwa na famiia unaoitwa Individualized Family Service Plan (IFSP).

**Huduma za Early Intervention**

Huduma za EIP zinaweza kutolewa nyumbani au katika mazingira ya huduma ya watoto, popote mtoto alipo.

IFSP inapitiwa kila baad aya miezi 6.

**Mapitio ya IFSP**

Mtoto wako anatathmini tena kila mwaka.

**Kuenda**

Elimu ya Watoto ya Mapema au Elimu Maalum ya Chekechea

**Mifano ya Huduma za Early Intervention ni pamoja na:**

- Tiba ya matamshi
- Tiba ya mwili
- Tiba ya shughuli za kila siku
- Ushauri wa familia

## Head Start (umri wa 0 hadi miaka 5)

Head Start na Early Head Start hutoa huduma na misaada kwa familia zinazostahiki ili kusaidia kutimiza malengo yao. Mipango hutoa machaguo ya siku nzima, nusu siku na ziara ya nyumbani bila gharama kwa familia.
Ili kupata mpango karibu nawe nenda kwenye:

**www.bit.ly/headstartprograms**




**Head Start Husaidia**
Masomo ya Mapema • Afya • Afya ya Akili
Elimu Maalum • Ustawi wa Familia




## Chekechea Inayofadhiliwa na Jimbo

(wa umri wa miaka 3 hadi 4)

Chekechea husaidia kuwatayarisha watoto kwa shule. Mipango inatolewa kupitia wilaya yako ya shule au mashirika yaliyo katika jamii bila gharama kwa familia yako. Wasiliana na wilaya yako ya shule kwa maelezo zaidi.

**www.bit.ly/earlylearningnys**

## Elimu Maalum ya Chekechea

(umri wa miaka 3 hadi 5)

Elimu Maalum ya Chekechea hutoa huduma ili kutimiza mahitaji ya wanafunzi wa chekechea waliotambuliwa kuwa na ulemavu. Huduma zinatolewa kupitia wilaya yako ya shule bila gharama kwa familia.

**www.bit.ly/specialednys**



**Elimuy Maalum ya Chekechea ni pamoja na Individual Education Program na mapitio ya kila mwaka:**

**1 IEP**
Individualized Education Program (IEP) imeundwa ili kutimiza mahitaji na malengo ya mtoto wako.

**2 Mapitio ya Kila Mwaka**
Kila mwaka, mkutano unafanywa ili kupitia maendeleo ya mtoto wako na kuamua malengo ya mwaka unaofuata.

# Mwongozo wa Familia kuhusu Huduma za Watoto za Mapema za NYS – Kabla ya Kuzaliwa hadi Miaka 5

Mwongozo wa huduma kwa familia kuungana na kuunganisha watoto kwenye huduma za watoto za mapema katika Jimbo la New York

## Msaada wa Familia

**Likizo Inayolipiwa**
NYS inatoa likizo inayolipiwa ya kazi iliyolindwa ili kupatana na mtoto aliyezaliwa, kumhudumia mpendwa aliye na maradhi mabaya, au kusaidia familia kuondoa shinikizo wakati mtu ameitwa kwenye huduma ya jeshi ng`ambo. Piga simu ya Usaidizi kwa **1.844.337.6303** au tembelea **www.bit.ly/paidleavenys**

**NYS Department of State, Office for New Americans**
Huwapa wahamiaji wote huduma za bila malipo na ni pamoja na waongozaji katika jamii, uundaji wa wafanyakazi, masomo ya lugha ya Kiingereza yanayotamba na huduma za kisheria. Piga simu **1.800.566.7636** au tembelea **www.bit.ly/onanys**

**NYS Office of Temporary and Disability Assistance, Enhanced Services to Refugees Program**
Husaidia familia mpya za wakimbizi zilizowasili kupata huduma kama vile mafunzo ya lugha, huduma za afya na ajira. Piga simu **518.402.3096** au tembelea **www.bit.ly/rsnys**

**Kinship Care**
Hutoa maelezo, rufaa na usaidizi kupitia tovuti yao **www.nysnavigator.org** na nambari ya simu bila malipo **1.877.454.6463**

**Prevent Child Abuse NY**
Hutoa msaada za kulea na huduma ikiwemo simu ya usaidizi kwa mzazi. Piga simu **1.800.244.5373** au tembelea **www.preventchildabuseny.org**

## Ulemavu wa Ukuaji

**Parent to Parent of NYS**
Huwezesha familia zinazowahudumia watoto walio na ulemavu wa ukuaji. Piga simu**1.800.305.8817** au tembelea **www.parenttoparentnys.org**

**Families Together of NYS**
Husaidia familia na watoto walio na matatizo ya jamii, hisia na tabia. Pigia simu **518.432.0333** au tembelea **www.ftnys.org**

## Afya ya Akili

**Ofisi ya NYS ya Afya ya Akili**
Hukuunganisha kwenye rasilimali na huduma za karibu za mfadhaiko wa kabla na baada ya kujifungua, afya ya akili ya mtoto na mahitaji mengine ya familia yako. Ikiwa uko kwenye mgogoro, unaweza kutuma ujumbe usiokutambulisha **GOT5** kwa **741741**. Pia unaweza kupiga simu **1.800.273.TALK (8255)** au tembelea **www.bit.ly/mentalhealthnys**

**Postpartum Resource Center of New York (Kituo cha Huduma za Baada ya Kujifungua cha New York)**
Huhakikisha kuwa familia zinapata msaada wa afya ya akili unaohitajika baada ya kujifungua Piga Simu ya Usaidizi kwa **1.855.631.0001** au tembelea **www.postpartumny.org**

## Misaada ya Uraibu

**Ofisi ya NYS ya Huduma na Misaada ya Uraibu**
Ikiwa wewe au mpendwa anatatizwa, unaweza kupata usaidizi na tumaini kwa kupiga simu, saa 24, siku 7 kwa wiki **1.877-8-HOPENY (1.877.846.7369)** au kutuma ujumbe **HOPENY** (Msimbo Mfupi **467369**). Kwa tiba ya uraibu, huduma ya mgogoro/uondoaji sumu, mgonjwa wa kulazwa, au asiyelazwa nenda kwenye **FindAddictionTreatment.ny.gov** au **www.bit.ly/oasasnys**

## Afya na Usalama

### Dhuluma za Nyumbani

**Ofisi ya NYS ya Uzuiaji wa Dhuluma za Nyumbani**
Ikiwa wewe au mtu unayemjua ni mwathiriwa wa dhuluma za nyumbani na unataka kusaidia, makao au maelezo ya dharura, wasiliana na mpango wa dhuluma za nyumbani katika jamii yako. **www.bit.ly/dvhelpnys** au piga simu ya Dharura ya Dhuluma za Nyumbani na za Mapenzi: **1.800.942.6906**, Upatikanaji wa Lugha ya Kiingereza na Kihispani/Lugha Nyingi. Asiyesikia au Aliye na Matatizo ya Kusikia: **711**.

**Growing Up Healthy Hotline**
Hutoa maelezo kuhusu huduma ya afya, lishe na mahitaji mengine ya familia. Inapatikana saa 24 kila siku, siku 7 kwa wili kwa Kiingereza, Kihispani na lugha nyingine. Simu zote ni za siri. **1.800.522.5006**

**Medicaid + Child Health Plus**
Familia yako inaweza kustahiki Medicaid au CHP ukitimiza matakwa fulani ya kifedha. Tuma ombi kupitia NY State of Health marketplace, au kwa kupigia Medicaid au CHP Helpline kwa nambari **1.800.698.4KIDS**

**NY State of Health Marketplace**
Huduma ya mtandaoni ya kukusaidia kununua, kulinganisha na kujisajili katika bima bora ya afya ya bei nafuu. **www.nystateofhealth.ny.gov**

**Huduma na Rasilimali za Meno**
Pata huduma za afya ya mdomo kabla ya kuzaliwa na za watoto. Pia simu **1.855.355.5777** TTY **1.800.662.1220** au tembelea **www.bit.ly/dentalnys**

**Uzuiaji wa Majeraha**
SAFE KIDS NY ni shirika lililojitolea kuzuia majeraha kwa watoto na lina miungano ya ndani. Piga simu **516.881.7000** au tembelea **www.bit.ly/safekidsnys**

## Mahitaji ya Msingi
### (Chakula mavazi, makao)

**WIC** (Mpango Maalum wa Lishe ya Ziada kwa Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto Wakubwa)
WIC huendeleza na kusaidia afya bora ya watoto wachanga, watoto wakubwa wanaostahiki na wanawake wajawazito, wanaonyonyesha au baada ya kujifungua. **www.bit.ly/wicnys**



**SNAP**
(Supplemental Nutrition Assistance Program)
SNAP husaidia kukukunulia wewe na familia yako chakula bora kwa afya. **www.bit.ly/snapnys**

**HEAP** (Home Energy Assistance Program)
HEAP husaidia kulipa gharama ya kupasha joto nyumbani kwako. **www.bit.ly/heapnys**

**Regional Food Bank**
Kwa usaidizi wa kuunganishwa kwenye hifadhi ya chakula ya karibu nawe tembelea tovuti ya Idara ya Afya ya NYS **www.bit.ly/foodbanknys**

**Msaada wa Makao**
Ikiwa huna makao kwa sasa au uko kwenye hatari ya kukosa makao, wasiliana na Department of Social Services (Idara ya Huduma za Jamii ya karibu nawe **www.bit.ly/housingnys**

**211nys**
**211** ni nambari rahisi ya kukumbuka ambayo husaidia kuunganisha familia za NY na mahitaji na misaada ya msingi

**Maelezo ya ustahiki na usajili kwenye Mipango ya Usaidizi, bima ya afya na mikopo ya ushuru yanaweza kupatikana kwenye* https://mybenefits.ny.gov/mybenefits/begin



## NYS PARENT PORTAL
**WWW.NYSPARENTING.ORG**

Download on the App Store | GET IT ON Google play

**Huunganisha wazazi kwenye tovuti bora kwa familia ikiwa ni pamoja na:**
- The NYS Parent Guide
- The NYS Child Care and After School Program Locator
- The Multiple Systems Navigator
- Every Student Present

## Wa Kuwasiliana Nao wa Karibu

**Daktari wa Watoto:**

**WIC Center:**

**Food Pantry:**

**Home Visiting Program:**

**Huduma za Watoto na Wakala wa Rufaa:**

**Early Intervention ya Kaunti:**

**Mratibu wa Early Head Start / Head Start:**

**Wilaya ya Shule:**

**Jisajili kwa Bima ya Afya:**
**www.nystateofhealth.ny.gov**
**1.800.541.2831**

**Udhibiti wa Sumu:**
**1.800.222.1222**

**Simu ya Ujumbe wa Mgogoro:**
**Tuma ujumbe "Got5" kwenye 741-741**

Kwa usaidizi wa Grant Number 90TP005902 kutoka U.S. Department of Health and Human Services, Administration for Children and Families, Office of Child Care. Maudhui yake ni wajibu wa waandishi na hayawakilishi maoni rasmi ya Office of Child Care, the Administration for Children and Families or the US. Department of Health and Human Services.

Ilirekebishwa 11/2021